



COUNTY ASSEMBLY OF MOMBASA
THE HANSARD

Tuesday, 4th March, 2025

Third Assembly – Fourth Session
FOURTH SITTING

*[The County Assembly met at 2:48p.m at the County Assembly Buildings]
[The Speaker (Honourable Aharub Ebrahim Khatri) in the Chair]*

PRAYERS

The Speaker (Hon. Khatri): Honourable Members, you may be seated. Yes, Clerk next order please.

MOTION

APPROVAL OF APPOINTMENT OF MEMBERS OF THE COUNTY ASSEMBLY NOMINATED BY
COUNTY ASSEMBLY PARTIES TO BE MEMBERS OF HOUSE BUSINESS COMMITTEE

Yes, Honourable Athman Mwamwiri, please move the Motion.

The Leader of Majority (Hon. Mwamwiri): Thank you, Mr. Speaker. Mr. Speaker Sir, I beg to move the following Motion.

That, pursuant to provisions of Standing Orders 151, subsection 1b, this Assembly approves the appointment of the following Members, nominated by the County Assembly parties, to be Members of the County Assembly Business Committee, in addition to those specified in Standing Orders 151, A, B, and C.

1. Hon. Priscilla Mumba.
2. Hon. Abrahman Hussain.
3. Hon. Mariam Baimu.
4. Hon. Frankline Makanga.
5. Hon. Mwinyi mtoto.
6. Hon. Hawa Abdulrahman.
7. Hon. Hawa Ibrahim Bomoa.
8. Hon. Kibwana Baya.
9. Hon. Milka Moraa
10. Hon. Naim Shafik

May I call Honourable Hamisi Salim Mbaya to second the Motion?

Hon. Hamisi Salim Mbaya: Thank you, Mr. Speaker Sir. I stand to second the Motion.

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you very much, Honourable Members. Honourable Members, I now propose the question that the Motion by Honourable Athman Mwamwiri on appointment of Members to the County Assembly Business Committee be considered by this Honourable House in the same terms as moved.

[Question proposed and agreed]

Yes, Honourable Athman Mwamwiri, please make your contribution to the Motion.

The Leader of Majority (Hon. Mwamwiri): Thank you, Mr. Speaker. Mr. Speaker, as provided in Standing Orders, upon returning from a long recess, this House, among the first businesses, it must approve a House Business Committee which shall necessitate the plans and businesses for this House, to take on. So, I urge all Honourable Members to approve this list of Members. All of them, Mr. Speaker served in the last session and they did well, in executing their mandate. I, therefore recommend that you approve them to proceed so that the House can now allocate business for the day to commence in this House. Thank you, Mr. Speaker.

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you very much. Yes, Honourable Mbaya.

Hon. Hamisi Salim Mbaya: Ahsante sana Mheshimiwa Spika kwa kunipatia fursa hii ili niweze kuchangia. Nimesimama kuunga mkono hoja hii Mheshimiwa Spika kawaida huwezi songa mbele mpaka uweze kujipanga na hauwezi kua na mipango kabambe mpaka uweze kujitayarisha na kutokana na wale ambao wamechaguliwa katika shughuli hii ni bora tuweze kuwapitisha kwa sababu ndio tuweze kujipanga na yale ambayo yako mbele yetu. Kwa hiyo nimesimama kuunga mkono hoja hii, ahsante sana Mheshimiwa Spika.

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you very much Honourable Mbaya. Yes, Honourable Fadhihi Makarani please make your contributions.

The Deputy Speaker (Hon. Makarani): Ahsante sana Mheshimiwa Spika. Mimi pia nimesimama kuunga mkono hoja iliyoletwa mbele na Kiongozi wa Walio Wengi kuhusiana na Kamati hii yetu ya Nyumba ambayo ndio inayopangilia mipangilio ya shughuli zetu za hapa Bunge. Mheshimiwa Spika, tukikumbuka ya kwamba mwaka tuliitoka nashukuru kwamba iliweza kupitia Kamati hii tuliweza kupitisha sheria nyingi pamoja na Miswada mingi katika Bunge hili hii, na ni kutokana na mipangilio mizuri ambayo Kamati iliyoondoka ilikua inafanya. Kwa hivyo Mheshimiwa Spika nawaomba wale wanao ingia katika kuchukua hatamu katika Kamati hii muweze kushirikiana na Waheshimiwa wenza ambao hawako katika hii Kamati ili tuhakikishe Bunge letu la Mombasa linaweza kufanya kazi zake kikamilifu. Pia vilevile Mheshimiwa Spika tunawaomba ambao watakao kua wamefaulu kuingia katika hii Bunge katika msimu huu ambao tunaendelea nao kwa msimu wa Ramadhani wakienda kukaa waweze kupangilia kwa zaidi maana twajua iko ratiba ambayo italetwa katika Bunge letu, ratiba ya Bunge letu baada ya hawa kukaa kwamba watakapokua wanapitia ile ratiba waweze kuangalia masuala haya ya mwezi huu mtukufu wa Ramadhan na vilevile Mheshimiwa Spika kuna ile *legislative counsel* pia twasikia iko njiani.

DISCLAIMER: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor Page 2*

Mheshimiwa Spika, tunaomba watakapokua wanaketi waweze kuangazia mambo haya na pia vile vile tumepokea stakabadhi nyingi kutoka ofisini za *Executive* ambazo moja ni hino CIDP kuna ADP ambayo inaendelea kuna CFSP ambayo ipo hizi zote mheshimiwa Spika ni changamoto katika Bunge letu maana pia nimeona kuna ratiba imetolewa ya vikao vya umma kuhusiana masuala ya ADP. Hizi zote Mheshimiwa Spika ni kazi ambazo zinakuja katika Bunge letu so naomba wake watakao kua wamekaa katika Kamati hii wawe ngangari zaidi na waweze kuhakikisha shughuli na taratibu za Bunge letu linaendelea kisawa sawa. Ahsante Mheshimiwa Spika na mimi naunga mkono.

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you very much Honourable Fadhili. Yes, Honourable Ahmed Khamis, please make your contributions.

Hon. Ahmed Khamis: Ahsante Mheshimiwa Spika. Nimesimama kuunga mkono mabadiliko muliofanya ya House Business na natumaini kua mabadiliko yatakua mengi katika Bunge hili.

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you very much. Yes, Honourable Mariam Baimu, please make your contributions.

Hon. Baimu: Ahsante sana Mheshimiwa Spika kwa kunipa nafasi hii. Mimi nimesimama kuunga mkono Mswada huu kuhusu pendekezo la watu walio orodheshwa katika hii Mswada waweze kuendeleza hiyo mipangilio ya nyumba katika ratiba za kupanga mikakati ya hili Jumba nimesimama kuunga mkono. Ahsante Mheshimiwa Spika.

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you very much. Yes, Honourable Juma Mwalimu, please make your contributions.

Hon. Juma Mwalimu: Ahsante sana Mheshimiwa Spika kwa kunipatia fursa hii mimi nimesimama kuunga mkono Mswada huu kwa sababu hawa waliochaguliwa ni wajuzi wale wa kuandaa Miswada kabla haijafika Bungeni kwa hiyo naunga mkono nawatakia kila heri na nawatakia Waislamu wenzangu Ramadhan Karim wa *Saum Makbul*.

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you Honourable Mwalimu. Yes, Mohammed Hamidi Khamis.

Hon. Mohammed Hamid: Ahsante sana Mheshimiwa Spika mimi naunga mkono moja kwa moja lakini niko na mambo mawili au moja lazima nizungumze hawa Waheshimiwa waliochaguliwa tunawaomba wawajibike na hii Kamati manake wengine twaona majina tu lakini wakati wa shughuli hatuwaoni. Kwa hivyo ni muhimu ukipewa nafasi ushughulike Mheshimiwa Spika; mimi sipingi lakini ukipewa nafasi ushughulike ukipewa nafasi wengine twawaona majina tu lakini wakati hizi Kamati zikifanya kazi hatuwaoni wakati Bunge waendelea hatuwaoni. Hata tumesahau kama wengine ni Waheshimiwa hapa kwa hivyo mimi ningeliomba hili jambo liangaliwe kwa karibu saa kwa sababu hii Kamati ni muhimu sana katika Jumba hili, ahsanteni sana.

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you very much. Yes, Honourable Hamida Noor.

Hon. Noor: Thank you, Mr. Speaker for giving me this opportunity to give my views on the Committee of House Business. As my colleague has just emphasized that the people who are in this Committee should be accountable on whatever is going to be brought to their Committee; for those few remarks I support.

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you. Yes, Honourable Florence please make your contributions.

Hon. Florence: Thank you Mr. Speaker this opportunity. I urge the newly appointed Members to work diligently for the betterment of MCAs. Thank you.

The Speaker (Hon. Khatri): Yes, Honourable Patrick Mbelle please make your contribution.

Hon. Mbelle: Shukran Mheshimiwa Spika. Kwanza niwapongeze Kamati hii kuweza kutumikia Jumba hili na wananchi wa Mombasa katika upangaji wa ratiba na yale yanatendeka katika Jumba hili. Langu pia ni kuwatia motisha ya kwamba tunapoelekea katika miaka hii miwili au miwili na ya mwisho kuna umuhimu wa kuweka kasi zaidi katika utendaji kazi katika Bunge hili. Kwa hivyo watie bidii watusaidie kutekeleza katika shughuli za hapa kwa manufaa ya wananchi wa Mombasa na kwa manufaa ya hata sisi Waheshimiwa ambao tuko katika Jumba hili. Ahsante Mheshimiwa Spika nauunga mkono.

The Speaker (Hon. Khatri): Thank very much. Yes, Honourable Leyla Nyache?

Hon. Nyache: Ahsante sana Mheshimiwa na mimi kuweza kuniona. Nimesimama kuunga mkono hoja hii iliyokuja na Mheshimiwa mwenza Mheshimiwa Athman Mwamwiri. Mheshimiwa Spika, nataka nichukue fursa hii niwapongeze walioteuliwa kuwa watakuwa katika hii Kamati ya *Appointment of Members* na ningewaomba waweze kuwajibika ndio kazi zetu ziweze kuwa rahisi na pia itaweza kuleta natija katika Mombasa yetu, ninawapongeza na kuwatakia kila la heri. Shukran Mheshimiwa Spika.

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you very much. Yes, Honourable Nusura Mwinyi?

Hon. Nusura Mwinyi: Ahsante Mheshimiwa Spika na mimi pia kuniona. Mimi nataka kusema nimesimama kuunga mkono; kwanza ukiangalia wale wote walioteuliwa hapa, nimeona pia aliyefanya kazi hii amezingatia jinsi pia tumeona wanawake wamewakilishwa hapa kikamilifu. Nataka pia niwaambie wale walioteuliwa hii ni Kamati ambayo ndio bora zaidi hapa katika Bunge hili ambayo inapanga biashara zetu za hapa ndani Bungeni. Kwa hivyo nataka niseme Mheshimiwa Mohamed Khamis amesema pale watu wanachaguliwa kisha hawaonekani hivyo basi mulioteuliwa kazi kwenu tunawategemea nyinyi. Nimesimama kuunga mkono.

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you very much. Yes. Honourable Shuhudia Abdallah?

Hon. Shuhudia Abdallah: Ahsante sana Mheshimiwa Spika kwa kunipatia fursa hii. Mimi nimesimama kuunga mkono hoja hii, pia nimesimama kuwapongeza wote walio chaguliwa na pia nawatakia kazi njema katika kazi yao hii waliochaguliwa. Shukran nimesimama kuunga mkono.

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you very much. Honourable Simon Mwaura please make your contribution.

Hon. Mwaura: Ahsante sana Mheshimiwa Spika kwa kunipa fursa na mimi nichangie katika swala hili linalohusiana na Kamati na Mipango ama Kamati ya Ratiba katika Bunge hili. Mheshimiwa Spika niwapongeze wale ambao wamepata hizi nyadhifa na niwaambie kwa kweli kama jinsi wenzangu walivyosema ni wakati wa kufanya kazi, ni wakati wa kuhakikisha nalo Bunge hili anga limewatumikiwa wananchi wa Mombasa kwa kipindi ambacho tumebakisha; kwa hivyo Mheshimiwa Spika ni wauunge mkono hawa ambao wamebahatika kuwa ama kuteuliwa katika Kamati hii ahsante.

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you very much Honourable Samwel Mwaura. Yes, Honourable Juma Manuari?

Hon. Juma Manuari: Ahsante Mheshimiwa Spika. Kwanza nichukue fursa hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa siku ya leo ya mwezi wa Ramadhani na tunamuomba Mwenyezi Mungu akubalie wale Waislamu walio funga saumu zao. Mheshimiwa Spika mimi nimesimama kama walivyo simama wenzangu nimesimama kuunga mkono ila nitakuwa na maneno mawili tu machache katika hoja hii iliyoletwa, angalau na sisi pia tuangalie ki upande mwingine haya maneno tutayaweka vipi? Kweli katika mipangilio wa orodha iliyotajwa hapa wameipangilia katika mpangilio mzuri wa kuzingatia jinsia lakini pia mbali na kuzingatia jinsia, Mheshimiwa Spika sijui utanieleza pengine kama itakuwa pana kasoro lakini kulingana na maeneo naona eneo la Likoni hapa limewakilishwa katika hizi Kanuni za kudumu No.151 (c) peke yake ndio, Kanuni za kudumu No.151 (b) ndio imeingia kama mtu wa Likoni kutokana na maeneo kwa sababu nikiangalia kuanzia mwanzo mpaka mwisho naona katika Sub County zetu za Likoni maeneo Bunge yetu ya Mombasa yote yamewakilishwa mara mbili, mara mbili, mara mbili.

Lakini katika eneo Bunge la Likoni tunaona tu kuna mwakilishi mmoja tu ambao ni kiongozi wa wengi ambao ameingia, wazungu wanasema *automatic* katika swala hili ambapo mimi Mheshimiwa Spika kutokana na mwelekeo na vile ninavyoona, ingekuwa bora pia katika hao watu kumi ambao wako chini angalau pia kupatikane mmoja wa Likoni mbali na yule ambaye ataingia hapo kama wazungu wanavyosema *automatic* katika msururu huu wa hawa ndugu zetu kwa hayo Mheshimiwa Spika mimi nimeuunga mkono japo nimetoa hoja yangu ya kurekebisha na tuangalie sisi watu wa Likoni kama tunavyojijua Likoni Sub County ndio inavukisha viongozi wengi pale feri kuja kupitisha swala hili na tunajua hii *Order Paper* yetu leo iliyotoka laiti itachukuliwa na wale wapinzani wetu, wale mahasimu wetu, ama wale watu wetu wa kule nyanjani wataanza kusema nyinyi Wabunge wa Likoni tunaona kazi yenu ni kwenda tu lakini mipangilio ya Nyumba munapangiwa na wengine. Kwa hayo mengi machache Mheshimiwa Spika, nimeuunga mkono hoja hii.

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you Honourable Juma Manuari. Yes, Honourable Allen Katana please make your contribution.

Hon. Katana: Mheshimiwa Spika nikushukuru kwa nafasi hii na nikizingatia kwamba saumu imenilemea sitaki kuwa na mchango mkubwa na si wakati wa kumjibu mtu. Lakini nimtoe kidogo wasi wasi Mheshimiwa Juma Manuari ya kwamba kwa kuwa Kamati hii ni ya kutuletea mipangilio ya hoja zitakazo kuwa zikiendelea hapa na kwa kuwa Jumba lote litahusika kwa kuhakikisha kinachopitishwa kinapitishwa kwa manufaa ya kila maeneo, mimi Mheshimiwa

Spika kwa nafsi yangu sina wasi wasi nao. Hata hawa wa Kisauni wakitoka wa Likoni wakiongezwa kisha nataka kuamini Mheshimiwa Spika kuwa kazi itafanyika. Mheshimiwa Spika, pia pengine Waheshimiwa wenza wengine wataniwia radhi lakini niongezee shime katika hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Mohamed Khamis Hamid ya kwamba majukumu haya tumewapa si kuwa muingie kwa kumbukumbu za Jumba hili ya kwamba mulipata nafasi ya kuhudumu kama hii. Mheshimiwa Spika niseme ya kwamba hiki ni kikundi cha watu ambao wana kazi muhimu katika Jumba hili Mheshimiwa Spika, mara nyengine inaudhi kugundua ya kwamba hatuna ajenda za kutuingiza hapa na ilhali Kamati kama hii ipo. Mheshimiwa Spika, ni kwamba ikiwa hata umepata uteuzi huu na una uhakika ya kwamba wewe ni baadhi ya wale ambao hupendi kuja Bunge tafadhali niseme itakuwa vizuri ukitupa ya barua ya kwamba nafasi hii nashukuru mumenipa. Lakini sitaweza kuifanyia kazi ile tuweze kumpa nafasi hii mtu ambaye atatusaidia ili tuweze kuhudumia watu wetu wa jimbo letu la Mombasa. Kwa hayo mengi niwatakie kila mtu Ramadhani Kareem na tunapoendelea kupambana kuwahudumia watu wetu wa Mombasa ahsante

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you very much Honourable Katana. Yes, any other Member who wants to contribute?

[Silence]

Yes, Honourable Athman please you may reply to the Motion.

The Leader of Majority (Hon. Mwamwiri): Ahsante Mheshimiwa Spika. Mheshimiwa Spika nishukuru Waheshimiwa wenza walioweza kuchangia lakini pia ikumbukwe ya kwamba hakuna mabadiliko katika uanachama wa Kamati hii, hawa wote walioweza kuhudumu katika Kamati iliyotangulia na nina imani kwa sababu utenda kazi wao imelazimu kuweza kurudi katika Kamati hii kwa sababu hatukuweza kupata ripoti ya malalamishi kutoka kwa wanachama ama Waheshimiwa kuhusiana na mmoja ama wawili wa wanachama walioko Kamati hii. Kumaanisha mwaka uliopita walitenda kazi yao barabara na ilipendeza wengi; lakini pia Mheshimiwa Spika nihimize ama niusie Waheshimiwa ya kwamba jukumu kubwa la Kamati hii ni kupangilia biashara zitakazo ingia katika Bunge hili na sio kuleta biashara zenyewe. Kwa hivyo ni jukumu la kila Mheshimiwa kwa ule muda tumekuwa katika likizo yale tuliyoweza kuyapata kutoka kwa watu wetu na maeneo yetu tuweze kuwatengenezea hoja kuweza kutengenezea Miswada ije katika Kamati na kupangiwa wakati itakapo jadiliwa katika Bunge hili. Hilo ndilo swala la Kamati hii, lakini Mheshimiwa Spika Kamati hii hata ikukutana mara mbili kwa siku kama hakuna biashara kutoka kwa waheshimiwa...

[Applause]

Hakuna watakachoweza kukipangia na kuingia hapa, kwa hivyo hima hima Mheshimiwa, Waheshimiwa binafsi tuwajibike Kamati zetu zingine tuweze kuwajibika zile ripoti zinazostahiki zifike kwa Kamati hii na kuweza kupangiwa wakati wa kuingia katika Bunge letu. Kwa hayo Mheshimiwa Spika nishukuru Waheshimiwa kwa changizo zao shukran.

The Speaker (Hon. Khatri): Thank very much Honourable Athman Mwamwiri. Honourable Members, I now put the question that the Motion by Honourable Athman Mwamwiri on *Appointment of Members to the County Assembly Business Committee* be adopted by this Honourable House in the same terms as moved.

[Question put and agreed to]

ADJOURNMENT

Honourable Members, this House stands adjourned until Wednesday 5th March, 2025 at 10:10a.m.

The House rose at 3:14p.m.